



(uten bilder)

- Zulu folktale
- Wiehan de Jager
- Brigid Simiyu
- swahili / bokmål
- nivå 4



Kisasi cha Kiongozi
Honningguidens hevn



Barnebøker for Norge

barneboker.no

Kisasi cha Kiongozi / Honningguidens
hevn

Skrevet av: Zulu folktale

Illustrert av: Wiehan de Jager


Oversatt av: Brigid Simiyu (sw), Espen Stranger-
Johannessen (nb)

Denne fortellingen kommer fra African Storybook (africanstorybook.org) og er videreformidlet av Barnebøker for Norge (barneboker.no), som tilbyr barnebøker på mange språk som snakkes i Norge.

Dette verket er lisensiert under en Creative Commons

[Navngivelse 3.0 Internasjonal Lisens.](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0/deed.no)

<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0/deed.no>



Hii ni hadithi ya Ngede, ambaye ni ndege mpenda asali, na mvulana mmoja mlafi anayeitwa Gingile. Siku moja Gingile alipokuwa akiwinda alisikia mwito wa Ngede. Kinywa chake kilianza kutokwa mate kwa kufikiria asali. Alisimama, akasiliza na kuangalia vizuri hadi alipomwona yule ndege akiwa ametua kwenye matawi yaliyokuwa juu ya kichwa chake. "Chitik-chitik-chitik," yule ndege mdogo alitatarika aliporuka na kutua kwenye mti mmoja hadi mwingine, na mwingine tena. "Chitik-chitik-chitik," aliita, huku akinyamaza na kuhakikisha kwamba Gingile alikuwa amemfuata.

...


Dette er historien om Ngede, honningguiden, og en grådig ung mann ved navn Gingile. En dag mens Gingile var ute på jakt, kalte Ngede på ham. Gingile fikk vann i munnen ved tanken på honning. Han stoppet og lyttet oppmerksomt, og lette til han så fuglen i grenene over hodet sitt. "Tsjitikk, tsjitikk, tsjitikk", kvitret den lille fuglen idet den fløy til det neste treet, og det neste. "Tsjitikk, tsjitikk, tsjitikk", kallet han, og stoppet innimellom for å forsikre seg om at Gingile fulgte etter.



Baada ya nusu saa, walifika kwenye mti wa matini. Ngede aliruka kama mwenda wazimu kutoka tawi moja hadi jingine. Kisha alitulia kwenye tawi moja na kupindua kichwa chake akimwanzia Gingile kana kwamba anasema, "Ipo hapa! Njoo sasa! kwa nini unachukua muda mrefu?" Gingile hakuweza kuona nyuki wowote kutoka chini ya mti, lakini alimwamini Ngede.

...


Efter en halvtimme nådde de et stort vilt fikentre. Ngede hoppet rundt som en gal blant grenene. Han slo seg ned på en gren og strakk hodet mot Gingile som om han sa: "Her er det! Kom nå! Hvorfor bruker du så lang tid?" Gingile kunne ikke se noen bier fra under treet, men han stolte på Ngede.



Kwa hivyo Gingile aliweka mkuki wake alioutumia kuwinda chini ya mti, akakusanya vijiti vilivyokauka na kuwasha moto mdogo. Moto ulipokuwa ukiwaka vizuri, alichomeka kijiti kirefu kwenye moto. Mti huu ulijulikana kwa kutoa moshi mwingi ulipokuwa unaungua. Alianza kukwea mti huku akishika kijiti kwa meno upande usiofuka moshi.

...


Så Gingile la spydet sitt ned under treet og samlet noen tørre kvister og tente et lite bål. Da ilden brant godt, stakk han en lang, tørr kjepp inn i hjertet av bålet. Denne veden var kjent for å lage mye røyk mens den brant. Han begynte å klatre mens han holdt den kjølige enden av kjeppen mellom tennene.



Muda mfupi baadaye, aliweza kusikia sauti ya nyuki
wenye harakati nyingi ikivuma. Walikuwa wakilingia na
kutoka kwenye upenyo wa mti, yaani mzinga wao.
Gingile alipoufika mzinga, alisukuma ile kuni ya moto
ndani ya ule upenyo. Nyuki waliharakisha kutoka ndani
wakiwa na hasira na uchungu. Waliruka na kwenda
mbali kwa sababu hawakupenda moshi – lakini walifanya
hivyo baada ya kumuuma Gingile kwa uchungu!

...


Snart kunne han høre summingen til de travle biene. De
kom inn og ut av et hulrom i trestammen – bolet deres.
Da Gingile nådde bolet, dyttet han den rykende enden
inn i hulrommet. Biene for ut, sinte og klare til angrep.
De fløy bort siden de ikke likte røyken – men ikke før de
hadde gitt Gingile noen smertefulle stikk!



Kwa hivyo wakati watoto wa Gingile wanaposikia hadithi
ya Ngede, wanamheshimu yule ndege. Kila wanapotoa
asali, huhakikisha kwamba wanamwachia kiongozi
fungu kubwa!

...


Og på den måten, når barna til Gingile hører fortellingen
om Ngede, respekterer de den lille fuglen. Hver gang de
sanker honning sørger de for å gi den største delen av
vokskaka til honninguiden!



Nyuki walipokuwa nje, Gingile aliingiza mikono yake ndani ya kiota. Alitoa kipande kikubwa cha sega kilichokuwa kinadondoka urojo mzito wa asali, na kilichojaa wadudu weupe wanene. Aliweka taratibu ndani ya mkoba aliokuwa nao na kuanza kushuka kutoka mtini.

...

Da biene var ute, stakk Gingile hånden sin inn i bolet. Han tok ut håndfuller med tunge vokskaker som dryppet av deilig honning og var fulle av feite, hvite larver. Han la vokskakene forsiktig i veska han bar på skulderen og begynte å klatre ned fra treet.



Kabla ya Chui kumvamia Gingile, alishuka chini haraka. Katika haraka hiyo, aliteleza na kuanguka kwa kishindo huku akiumia mguu wake. Alirukaruka akienda kwa haraka alivyoweza. Kwa bahati nzuri, Chui alikuwa bado amelala kwa hivyo hakumfukuza. Ngede, Kiongozi alikuwa amelipiza kisasi chake na Gingile alikuwa amejifunza funzo lake.


...

Før Leopard kunne svinge labben etter Gingile, skyndte han seg ned fra treet. I hastverket bommet han på en gren og landet med et høyt brak på bakken og forstuet ankelen. Han hinket videre så fort han kunne. Heldigvis for ham var Leopard fortsatt for søvnig til å jage ham. Ngede, honningguiden, hadde fått sin hevn. Og Gingile hadde fått seg en lærepenge.

Gingile alipopanda, alishangaa kwa nini hakusikia sauti ya nyuki. "Pengine mzinga umo ndani zaidi katika mti," alifikiria. Alipanda tena juu ya tawi jingine. Lakini badala ya mzinga, alijikuta uso kwa uso na chui! Chui alikuwa na hasira sana kwa sababu usingizi wake ulikuwa umekatizwa. Aliyafanya macho yake kuwa madogo, akaufungua mdomo wake na kuonyesha meno yake makubwa na makali.

...


Gingile klatret, men lurte på hvorfor han ikke hørte den sedvanlige summingen. "Kanskje bolet er dypt inne i treet", tenkte han for seg selv. Han dro seg opp etter en annen gren. Men i stedet for bolet, stirret han inn i øynene til en leopard! Leopard var veldig sint fordi søvnen hennes ble så brått avbrutt. Hun knep igjen øynene og åpnet munnen for å vise de veldig lange og skarpe tennene sine.




Ngede alishuhudia kila kitu Gingile alichofanya. Alikuwa anamsubiri abakishhe kiasi kidogo cha asali kama shukurani kwa kiongozi. Ngede aliruka kutoka tawi hadi tawi huku akikaribia chini. Mwishowe Gingile alifika chini ya mti. Ngede alitua kwenye mwamba karibu na mvulana huyo na kusubiri zawadi yake.

...

Ngede så ivrig på alt Gingile gjorde. Han ventet på at han skulle legge igjen en tjukk vokskake som en takkegave til honningguiden. Ngede svinset fra gren til gren, nærmere og nærmere bakken. Til slutt nådde Gingile foten av treet. Ngede satt på en stein nær gutten og ventet på belønningen sin.






Lakini Gingile alizima moto, akachukua mkuki wake na kuanza safari kwenda nyumbani bila kumjali ndege yule. Ngede aliita kwa hasira, “USH-ndi! USH-ndi!” Gingile alisimama, akamkodolea macho yule ndege kisha akacheka kwa sauti. “Unataka asali kidogo, rafiki yangu? Ha! Lakini ni mimi niliyefanya kazi yote pamoja na kuumwa na nyuki. Kwa nini nikugawie hii asali tamu?” Baada ya kusema hivyo, aliondoka na kwenda zake. Ngede alikasirika sana! Hivi sivyo alivyostahili kutendewa! Ila atalipiza kisasi.

...

Men Gingile slukket bålet, plukket opp spydet, begynte å gå hjem og overså fuglen. Ngede ropte sint: “SEI-er, SEI-er!” Gingile stoppet og stirret på den lille fuglen og lo høyt. “Du vil ha litt honning, du, lille venn? Ha! Men jeg gjorde alt arbeidet og fikk alle stikkene. Hvorfor skulle jeg dele noe av denne deilige honningen med deg?” Ngede var rasende! Dette var da ingen måte å behandle ham på! Men han skulle få sin hevn.



Siku moja baada ya majuma machache, Gingile tena alisikia mwito wa asali kutoka kwa Ngede. Aliikumbuka asali tamu, na kwa hamu alimfuata ndege yule kwa mara nyingine. Baada ya kumwongoza Gingile pembeni mwa msitu, Ngede alisimama na kupumzika chini ya mti wa mwavuli. “Ahh,” Gingile aliwaza. “Lazima mzinga umo ndani ya mti huu.” Kwa haraka aliwasha moto wake na kuanza kukwea mti huku akibeba kuni iliyotoa moshi katika meno yake. Ngede alikaa na kuangalia tu.

...

En dag flere uker senere hørte Gingile igjen kallet fra Ngede. Han husket den deilige honningen og fulgte ivrig etter fuglen nok en gang. Etter at den hadde ledet Gingile langs skogkanten, stoppet den for å hvile i et stort akasietre. “Å”, tenkte Gingile. “Bolet må være i dette treet.” Han tente raskt det lille bålet sitt og begynte å klatre med den rykende grenen mellom tennene. Ngede satt og ventet.